TANGAZO LA SERIKALI NA. 712 la tarehe 02/ 12/2022

SHERIA YA MIPANGOMIJI,

(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1))*

AMRI YA KUPANGA ENEO LA TUTUO YA MWAKA, 2022

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kupanga Eneo la Tutuo ya Mwaka, 2022.

Kutangazwa kwa eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipangomiji.

Mpango wa jumla na kina wa eneo

3. Mpango wa jumla na wa kina wa eneo lililoainishwa katika Jedwali unaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge.

## JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la Upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:

“Unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji T1 iliyopo katika makutano ya barabara ya Sikonge na Mto Kamdihu yenye majira-nukta 465543E, 9389448N; baada ya hapo mpaka utaelekea Magharibi kwa kufuata bonde la mto Kamdihu hadi alama T2 iliyopo katika makutano ya barabara ya Mpanda na bonde la Mto Kamdihu yenye majira-nukta 463201E, 9388867N; baada ya hapo mpaka utaelekea Kaskazini - Magharibi katika uelekeo wa N98$^{0}$6’32”W kwa umbali wa kilomita 4.9 hadi katika alama ya mpaka ya upimaji T3 iliyopo barabara ya Mitoo yenye majira-nukta 461187E, 9393285N karibu na mlima Mitoo; baada ya hapo mpaka utaelekea Kaskazini katika uelekeo wa N165$^{0}$11’0” kwa umbali wa kilomita 2.4 hadi katika alama ya mpaka ya upimaji T4 iliyopo barabara ya Urambo yenye majira-nukta 461112E, 9395237N; baada ya hapo mpaka utaelekea Mashariki katika uelekeo wa E89$^{0}$5’56” kwa umbali wa kilomita 4.7 hadi alama ya

mpaka ya upimaji T5 iliyopo barabara ya Tabora yenye majira-nukta 465750E, 9395072N, baada ya hapo mpaka utaelekea Mashariki - Kusini katika uelekeo wa E120$^0$8’9”S kwa umbali wa kilomita 1.25 hadi alama ya mpaka ya upimaji T6 yenye majira-nukta 466545E, 9393991N; baada ya hapo mpaka utaelekea Kusini katika uelekeo wa S150$^0$10’0” kwa umbali wa kilomita 5.08 hadi alama ya mpaka ya upimaji T7 iliyopo bonde la Mto Kamdihu yenye majira-nukta 466461E, 9389573N; baada ya hapo mpaka utafuata bonde la Mto Kamdihu hadi ulipoanzia”.

Dodoma,
8 Novemba, 2022

ANGELINE S. MABULA
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*